# VAENI SILAHA ZA NURU

Na Jacquelyn Fedor

Ilitafsiriwa Na David Odhiambo

**Isaya 11:6-9**

6 "mbwamwitu ataishi pamoja na mwanakondoo, chui watapumzika pamoja
na mwanambuzi. Ndama na mwanasimba watakula pamoja, na mtoto
mchanga atawaongoza.
7 Ng'ombe na dubu watakula pamoja, ndama wao watapumzika pamoja; na
simba atakula majani kama ng'ombe.
8 Mtoto mchanga atacheza kwenye shimo la nyoka, mtoto ataweza kutia
mkono shimoni mwa nyoka wa sumu.
9 Katika **mlima takatifu wa mungu** hakutakuwa na **madhara** wala
**uharibifu**. Maana **kumjua Mwenyezi-Mungu** kutaenea **pote nchini**, kama
vile maji yajaavyo baharini.

Hii ni picha nzuri ya ufalme wa Wanyama na vile ubinadamu unarejeshwa!

Hebu tuangalie **Ufunuo 21:1-5** tuone urejesho tena.

1 Kisha nikaona **mbingu mpya** na **dunia mpya**, kwa maana **mbingu ya**
**kwanza** na **dunia ya kwanza zimekwisha kupita** pia **hakukuwa na bahari**
(bahari ya wanadamu waovu).
2 Kisha mimi, Johana nikaona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka
lutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umetayarishwa vizuri kama bibi arusi
aliyepambwa tayari kukutana na mumewe.

3 Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka katika kiti cha enzi ikisema, “**Tazama**! **Maskani ya Mungu** iko **kati ya wanadamu**. **Atakaa kati yao**, nao **watakuwa watu wake**, **Mungu mwenyewe** atakuwa nao na **atakuwa Mungu wao.** (yote yatakuwa kamilifu na kurejeshwa).
4 Na **Mungu** atafuta **kila chozi** katika macho yao; **hakutakuwa na kifo tena**, wala **huzuni**, wala **kilio**. **maumivu** hayatakuwapo tena, kwa **maana mambo ya kwanza** yamekwisha **kupita**.”
5 Kisha yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, “**Tazama**, **nayafanya yote kuwa mapya** . Naye akaniambia, “Andika, kwa kuwa **maneno haya** ni ya **kweli na ya uaminifu**.”

Kwa wale ambao hawana uwezo wa kimwili au walemavu kwa njia yoyote ile, hii ni baraka nzuri sana ya kutazamia kwa hamu, hata hivyo, ili ahadi hizi zitimie, ni lazima tuelewe Warumi 8:29.

**Warumi 8:29**

29 Maana hao aliowachagua tangu mwanzo, ndio aliowateuwa wapate kufanana na mwanae, ili mwana awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

Baada ya kusoma maandiko hayo, cha kufikiria ni hii. Kwa kuwa Bwana alipanda kwa mkono wa kulia wa Mungu kutoa dhabihu ya mwili wake kwa ajili yetu, hana tena mwili wa kidunia, kwa hivyo, kwa sisi kufanana n asura yake, maandiko yanazungumza juu yake kama mtu wa mbinguni.

**1 Wakorintho 15:45**

45 Maana maandiko yasema: “**Mtu wa kwanza, Adamu**, alikuwa **kiumbe mwenye uhai**;” **Lakini Adamu wa mwisho** (Yesu) ni **Roho awapaye watu uhai**.

Kwa hiyo inakuwa dhahiri kwamba ni mwanadamu wetu wa kiroho pekee ndiye anayeweza kufananishwa na sura yake.

**1 Wakorintho 15:50**

50 Basi, ndugu, nasema hivi: kuwa **mwii na damu** haiwezi **kuuridhi ufalme** wa Mungu; wala chenye kuharibika hakiwezi kuridhi kutoharibika. (Ni waliozaliwa mara ya pili tu, waliojazwa na Roho, hivyo roho zetu huamshwa kwa Roho wa Mungu.)

Hii inaleta tatizo halisi kwani tunachojua ni maisha katika ulimwengu wa Shetani. Ujuzi wake kwa sehemu kubwa hujaza hifadhidata yetu, ambayo ni kinyume kabisa na maarifa na hekima ya Mungu. Kwa kuwa Kristo ni Neno, maarifa ya Mungu, ni jinsi gani tunapaswa kuwa katika sura yake iliyojaa maarifa ya Shetani!

Lakini Mungu anaahidi atatukamilisha yeye binafsi. Hakuna njia iwezekanayo tunaweza kufikia ukamilifu tukiwa na hekima ya Shetani kuwa mwongozo wetu.

**Wafilipi 1:6**

6 nikitumaini neno hili, ya kwamba **yeye** aliyeanza **kazi njema** mioyoni mwenu **ataimaliza** hata siku ya Kristo Yesu;

Na kwa kuwa ni Yeye aliyesema ya kwamba angetufananisha tena na sura na mfano wa Kristo, mnaweza kuona kile hasa anachozungumzia hapa ni roho yetu, nia zetu, mioyo yetu, nafsi zetu, utu wetu wa ndani, kwa kuwa hivyo ndivyo Kristo alivyo sasa. Ni wazi kuwa kama Yeye, dhambi pia lazima iondolewe kutoka kwetu.

Kwa bahati mbaya wengi wetu tunapofikiria kuhusu Upatanisho, au toba ya dhambi tunafikiri hasa kuhusu kile ambacho tumedhihirisha kupitia miili yetu, na hivyo tunatubu kila kitu tunachoweza kufikiria ambacho tumefanya vibaya katika maisha yetu yote. Lakini kwa hakika kile ambacho Mungu anapendezwa nacho kwanza ni kutakaswa kwa mioyo na akili zetu. Anapowatazama ni matumaini yake na yetu haoni giza lolote hapo. Uchunguzi huu unaouona huamua hali ya mtu wetu wa kiroho, au utu wetu wa ndani jinsi ulivyofanyizwa na kufinyangwa na kile kilicho katika akili na mioyo yetu.

**2 Wakorintho 4:16** inatuonyesha mtu wa ndani na mtu wa nje.

16 Kwa hiyo hatulegeiU Ingawa **utu wetu wa nje** unaharibika, lakini **utu wetu wa ndani** unafanywa upya siku baada ya siku.

Kwa hivyo, tuanze na akili zetu. Je, ulitambua kwamba dhambi ya kwanza kabisa ambayo mwanadamu alifanya ilikuwa akilini mwao? Wengi wetu tumesikia msemo,"tulikuwa na mkutano wa akili", na ndivyo ilivyotokea. Hawa aliunganishwa na akili ya Shetani! Alifikiria juu ya ujuzi ulioongezwa wa uovu aliopewa, hekima iliyopotoka ambayo Shetani aliwasilisha kwa hila. Moyo wake mkamilifu, ulioumbwa kuwa mwadilifu kabisa, ukawa mwovu na mwasi. Jinsi gani? Kwa nini? Kwa sababu alikula tunda lililooza kutoka kwa akili ya Shetani. Adamu, aliumbwa mwenye haki pia, hakudanganywa kama Hawa, bali alikuwa na mkutano wa akili na mke wake, kwa hiyo pia alikula tunda lililochafuliwa la ujuzi wa Shetani. Kama tunavyojua wote walianguka kutoka Paradiso na kuingia katika ulimwengu wa Shetani na wanadamu wote wamefuata mfano huo. Sasa leo ujuzi pekee unaopatikana kwetu kwa sehemu kubwa ni ujuzi ambao Adamu na Hawa walichagua na kwa bahati mbaya akili zetu zote zimechafuliwa vile vile na mawazo ya Shetani! Tumezoea kula matunda yake.

Maarifa haya yalipochukuliwa katika akili za mwanadamu, tabia ziliundwa, mawazo yaliwekwa na kuwa magumu kuondoa. Asili mbovu ya Shetani kupitia ujuzi wake imetupotosha sisi sote, na cha kusikitisha ni kwamba sisi sote hatujapatana kabisa na ulimwengu wa Mungu, pamoja na viumbe Wake wengine ambao Adamu na Hawa walipewa mamlaka juu yao. Uumbaji haukuwa na chaguo katika jambo hilo.

**Warumi 8:20**

20 Kwa maana **viumbe viliwekwa chini ya ubatili**, **si kwa hiari yao**, bali kwa ajili yake **yeye aliyeviweka katika tumaini**; (Kwa matumaini wanadamu wangefikia kuelewa hawawezi kufanya lolote bila Neno, ujuzi Wake, Kristo, kwani uliruhusu ujuzi na asili ya Shetani kuathiri yote ambayo Yeye alikuwa amempa mwanadamu.)

Ndiyo, Baba alikuwa na tumaini tungeweza kuona upumbavu wa kutochagua Neno badala ya Shetani. Vitu vyote viliumbwa ndani yake, Yeye ndiye kiumbe kinachoshikilia ulimwengu wote pamoja kwa hivyo bila Yeye hatuwezi kufanya chochote.

**Wakolosai 1:17**

17 Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na **vitu** vyote **hushikana katika yeye**. (vimeshikiliwa pamoja)

Inasikitisha kwamba kwa sababu ya kula matunda ya ujuzi wa ulimwengu mioyo ya wanadamu wengi imekuwa migumu dhidi ya Muumba wao. Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa ni ujuzi wa Shetani tu katika hifadhidata yao, mioyo na akili za mwanadamu zilifananishwa kwa urahisi na nguvu zinazoendesha ulimwengu huu pia. Asili ya Shetani inatawala.

Tamaa ya jicho, tamaa ya mwili, kiburi cha uzima ni nguvu zinazotawala za ulimwengu wa Shetani. kishawishi yao umeunda hali ya moyo ya watu wengi

ulimwenguni leo. Mauaji, upotovu, hasira, husuda na uchoyo kwa kutaja machache, ni matunda ya pepo wachafu wanaoishi katika mioyo ya wengi pia. Wao ni matokeo ya hekima na maarifa ambayo jozi ya kwanza walichagua. Tunaweza kuona wazi hitaji la akili na mioyo yetu kufanywa upya, kuwekwa huru kutokana na dhambi, kabla ya roho na utu zetu kuwa katika mfano wa Kristo!

Roho Mtakatifu anapoleta nuru mambo tunayohitaji kutubia, tunakua kweli kuelewa uzuri wa kile kilichotimizwa msalabani kwa ajili ya wanadamu na viumbe vyote! Je! unaweza kuona jinsi yote yangepotea kama si Yeshua! Aliteseka kwa ajili ya uovu na dhambi ya viumbe vyote, na alilipa adhabu ya kifo kwa ajili yetu. Ninasema uumbaji wote, kwa sababu kama tulivyojadili hapo awali, Adamu na Hawa walipoanguka, kila kitu walichokuwa na mamlaka juu yao kilianguka pamoja nao, na tabia za Shetani ziliingia ndani yao na vile vile mwanadamu. Ufalme wa wanyama, ikiwemo ndege na samaki wakawa wanyama wanaokula nyama (wala nyama), hatari kwa kila mmoja! Kama tulivyoona katika Isaya 11, haya yote yatarekebishwa siku moja kwa ufalme wa wanyama, na kama tulivyoona katika Ufunuo 21, kwa sababu ya ushindi kwenye msalaba, wanadamu watarejeshwa vilevile na hakutakuwa na uharibifu au kifo!

Je, mabadiliko haya yatatokeaje? Tunapochukua Neno, nuru inayotoka humo itafichua yale ambayo yamefichwa katika giza la mioyo na akili zetu kama yamepandwa na ujuzi wa Shetani.

**Danieli 2:22**

22 **Yeye** (Mungu) hufunua **mambo ya kina** na **ya siri**; **Anayajua** yaliyo **gizani**, na **nuru hukaa kwake**.

Wale walio na upendo wa kweli kwa Mungu watakaribisha nuru wanapoendelea kula ujuzi wa Mungu na wataanza kubadilika. Sote tuna hamu ya kurejeshwa na Malaki 4 inafunua ni lini jambo hili litatimia.

**Malaki 4:2**

2 Bali **kwenu nyinyi mnaolicha jina langu**, **Jua la Haki** l**itawazukia**, lenye **kuponya** katika mbawa zake; nanyi mtatoka na kunenepa kama ndama waliolishwa.

Kama tunavyoona katika neno, JUA ndiyo huleta uponyaji au urejesho. Kwa hivyo tukitegua kitendawili hiki cha kiroho ukipenda kwa kuangalia maandiko haya machache yanayofuata.

Hebu tuangalie kwanza **Yohana 14:20**.

20 Siku hiyo (siku ya nane) mtajua ya kuwa **mimi** niko ndani ya **Baba** yangu, **nanyi** ndani **yangu**, **nami ndani** **yenu**.

Sasa na tuangalie **Wakolosai 1:27.**

27 Kwao (watoto wa siku ya nane) Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa **siri hii** kati ya Mataifa, nao ni **Kristo** **ndani yenu,**

**tumaini** la utukufu.

Kwa hiyo Neno, Mwana wa Mungu yu ndani yetu nasi tumo ndani Yake!

Je! unakumbuka tulichojifunza katika **Wakolosai 1:17**?
17 **Naye amekuwako kabla ya vitu vyote**, **na vitu vyote hushikana ndani**
**yake** (au vimeundwa, au vimetengenezwa, amevishikilia).

Kwa hiyo vitu vyote vilivyoumbwa kupitia Yeye ni sehemu Yake na mahali pa asili viliposhikilia katika ulimwengu vitarudishwa kwao.

Kwa hiyo tukiwa na hili akilini sasa tuangalie **Mwanzo 1:14-16**.
14 Kisha Mungu (Baba) **akasema**, "**Na iwe mianga** katika anga la
mbingu ili kutenganisha mchana na usiku; nayo iwe kwa ishara na
majira na siku na miaka,
15 nayo iwe mianga katika anga la mbingu **itie nuru juu ya dunia**;"
ikawa hivyo.
16 Kisha Mungu (kupitia Mwanawe) akatengeneza mianga miwili
mikubwa: ule mkubwa utawale mchana (jua), na ule mdogo utawale
usiku (mwezi). Aliziumba nyota pia.

Baba alikuwa anazungumza na Mwanawe, na Mwanawe Yeshua alifanya jambo hilo litendeke. Nuru iliyotoka Kwake kweli iliumba jua, na nuru iliyoakisi kutoka kwenye jua iliumba mwezi.

Kumbuka sasa andiko lililosema, Baba yu ndani yangu, mimi ni ndani yenu, nanyi mko ndani yangu, katika 1 Yohana? Sasa tunaweza kuona, Mwana yule yule aliyeumba jua na mwezi mbinguni yuko ndani yetu!

Kwa hiyo wakati giza la dhambi linapoondolewa katika akili zetu na mioyo yetu, Mwana wa Mungu ndani yetu anaweza tena kuakisi nuru yake, akiumba jua la dunia ndani yetu! Pia, jinsi akili na mioyo yetu ilivyo safi na isiyo na giza lo lote, tunapopata ushirika tunakuwa kweli wamoja na Mkate wa Uzima, Tunakuwa kihalisi sehemu ya mwili Wake pamoja na Bibi-arusi Wake wa agano. Bibi-arusi anapopokea nuru kutoka kwa Mwana wa Mungu kwa vile sasa wao ni mwili mmoja, nyama ya nyama Yake, mfupa wa mfupa Wake, uhai wao unakuwa mmoja katika damu naye anakuwa mwezi wa nchi kavu.

**Luka 11:36**

36 Basi, **kama** mwili wako wote **una mwanga**, bila kuwa **na sehemu yeyote yenye giza**, **mwili huo** utakuwa **kamilifu** kama vile taa inavyokuangazia kwa mwanga wake." (Huu ndio urejesho kamili.)

Si wote watakaoamini ukweli huu wa wakati wa mwisho, wengine watadhihaki maarifa ya Mungu kwa sababu ni tofauti sana na yale ambayo ulimwengu unafundisha. Andiko itatuambia ni kwa nini.

**2 Wakorintho 4:4-6**

4 Hao **hawaamini** kwa sababu yule **mungu wa ulimwengu huu** (shetani)
**amezitia giza akili zao** wasipate kuuona wazi mwanga wa habari njema
(neno la Mungu) ya utukufu wa kristo, ambaye ni **mfano kamili wa Mungu**,
anafaa **kung'aa kwao**.
5 Maana hatujitangazi sisi wenyewe, ilatunamhubiri Yesu Kristo aliye
Bwana, sisi wenyewe tukiwa watumishi wenu kwa ajili ya Yesu.
6 **Mungu** ambaye alisema, "**Mwanga na uangaze kutoka gizani**," ndiye
mwenye **kuiangaza mioyo yetu**, na kutupatia **mwanga** wa **ujuzi** wa
**utukufu wa Mungu** uangazao katika **uso** wa **Yesu Kristo**. (tumesoma katika
maandiko ya awali kuwa Kristo yuko katika mfano wa Mungu.)

Kama tulivyojifundisha katika mafundisho ya awali, wakati kwa ukamilifu wa nafsi zetu, tutakuwa onyesho la hadithi ya Kristo angani, dhihirisho la ushindi wake na kurudi katika usawa uumbaji wa yesu hapo awali! Unaona, hadithi hii imekuwa mbinguni kwa mwanadamu kuuona tangu uumbaji wa Adamu na Hawa. Ingawa hadithi hii imefunuliwa mwanadamu miaka hii yote, wachache tu ndio wameelewa. Unaona jinsi mwanadamu leo wanakamilishwa, tutakuwa picha kamili ya Kristo. Kumbuka, ni picha kamili ya Mungu. Sisi, pamoja na hadithi angani, kwa wakati huu tutakuwa tumefahulu kutangaza maarifa yake kote duniani kama maji inavyo funika bahari ya binadamu katika utimilifu wa Mathayo 24:14.

**Mathayo 24:14**

14 Na injili hii ya ufalme itahubiriwa **katika ulimwengu wote** kama ushahidi kwa mataifa yote, na ndipo **mwisho utakapokuja**.

Tutakuwa tayari kwa urejesho kama ilivyoelezewa katika Isaya 11 na uumbaji wote wa Ufunuo 21 na tutakuwa tumedhihika kama wana wa Mungu, na uumbaji wote watakuwa na furaha wakiwekwa huru.

**Warumi 8:21**

21 kwa sababu **viumbe vyenyewe** navyo **vitakombolewa** **kutoka katika utumwa wa uharibifu** (hakuna kifo) hadi katika **uhuru wa utukufu** wa **watoto wa Mungu**.

Unaona, vitu vyote mbinguni na duniani mwishowe vitakusanywa ndani yake na kuwa sehemu ya nzima na sisi pamoja naotutakuwa sehemu ya nzima vile vile, sehemu ya ulimwengu.

**Waefeso 1:10**

10 Katita utimilifu wa nyakati (wakati Baba anaposema, inatosha kwa ulimwengu wa Shetani) apate **kukusanya pamoja** **vitu vyote** katika **Kristo** (kumbuka hadithi iko angani), **vyote** vilivyo **mbinguni** (ni sehemu ya uumbaji wote), na **vilivyo duniani** (kumbuka sisi ni mfano wa hadithi mbinguni); **hata katika** **yeye**;

Kwa hivyo tunaweza kuona ikiwa tutakusanywa ndani yake, jinsi lazima

tuwe safi! Akili safi, roho yetu yote, nasfi yetu yote lazima iwe mwonekano wake kwani yeye ni mwonekano wa Mungu, Watoto ya nuru, wachukuaji nuru.

**Danieli 12:3** alitabiri haya
3 **Walio** na **hekima** (wenye ujuzi wa Mungu) **watang'aa** kama **mng'ao** wa **anga**, (jua, mwezi) na wale wanaogeuza wengi kwenye uadilifu (wanaoeneza maarifa ya Mungu kote duniani kama maji yanavyofunika bahari) **kama nyota** (bingu na dunia zote zinasimulia hadithi) milele na milele.

Tunawaona tena katika **Matendo 13:47**.
47 Kwa maana ndivyo Bwana alivyotuamuru: 'Nime**kuweka** uwe **nuru** ya **mataifa**, ili **uwe wokovu** hata **miisho ya dunia** (kama vile maji yaifunikavyo bahari)."

Acheni tumalizie kwa andiko ili kuleta maanani ujumbe huu na kujibu fumbo linalopatikana katika Malaki 4.

**Warumi 13:12**
12 **Usiku** **umeendelea sana** (wakati unakaribia kwisha), **mchana umekaribia** (siku ya hukumu ya Bwana). Kwa hiyo **na tuyavue matendo ya giza,** na kuvaa **silaha za nuru**.

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com